**PROPER PREPARATION PREVENTS POOR PERFORMANCE**
**( PENTA)**

# PENTA TANZANIA


meshackstanley43@gmail.com
+255 764 760 769
KIHONDA- AZIMIO, MOROGORO


darasahuru.co.tz

# MTIHANI WA KWANZA WA UPIMAJI DARASA LA SABA
# KISWAHILI

**MUDA: SAA 1:00** **MACHI 2024**

**MAELEKEZO**

- **Mtihani huu una jumla ya maswali 35.**
- **Jibu maswali yote kwa usahihi katika kila sehemu.**
- **Zingatia usafi wa kazi yako.**
- **Kumbuka kuandika jina lako kwa usahihi.**
- **Kumbuka kuzingatia maelekezo ya kila sehemu na kila swali.**
- **Ukigundua kuwa herufi uliyoichagua sio jibu sahihi kata mara moja na uandike upya pembeni.**
- **Simu za mkononi, vikokotozi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

## SEHEMU A: UFAHAMU WA KUSIKILIZA, SARUFI, MSAMIATI NA FASIHI

**1. Sikiliza kwa makini hadithi utakayosomewa na msimamisi, kisha jibu swali la i – v kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.**

i. Maganga alikuwa kijana mwenye sifa nzuri zilizowavutia wanakijiji. Ni ipi kati ya sifa zifuatazo haikuwa sifa ya Maganga?
A. Alipenda maendeleo
B. Hakupenda kupiga vita ufisadi
C. Alipenda uwazi na hakupenda mzaha
D. Hakuwa na lugha ya kubembeleza katika kazi
E. Alikuwa jasiri na mwenye msimamo

ii. Nini maana ya msemo "ibuka kidedea" kama ulivyotumika katika habari uliyoisikiliza?
A. Kushindwa
B. Kushinda
C. Kupigiwa kidedea
D. Kuongoza kijiji
E. Kupigania haki

iii. Viongozi wa kijiji tanjwa katika habari uliyoisikiliza walipatikana kwa njia gani?
A. Kwa kuteuliwa na wanakijiji
B. Kwa kupendekezwa na wanakijiji
C. Kwa kuteuliwa na raisi
D. Kwa kutangazwa na bwana Jumbe
E. Kwa kupigiwa kura na wanakijiji

iv. Ni nani kati ya wafuatao hakuwa mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa kijiji?
A. Mzee Lukuminga
B. Bwana Jumbe
C. Maganga
D. Mzee mdula
E. Mzee mtasha

v. Kijiji gani kilifanya uchaguzi wa viongozi?
A. Kijiji cha muungano
B. Kijiji cha Songa mbele
C. Kijiji cha kalemela
D. Kata ya Muungano
E. Kijiji cha maendeleo

**2. Chagua jibu sahihi kisha jibu swali kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.**

i. Kijana huyu hapendi mzaha kabisa anapofanya kazi zake. Je, neno **mzaha** linamaanisha nini?
A. Utani
B. Uvivu
C. Michezo
D. Uzembe
E. Dharau

ii. Mzee Jongo alitaka mzee Mwendapole alipe fidia ya shilingi elfu hamsini kwa sababu kuku wake aliibiwa na mtoto wa mzee huyo. Je, neno fidia lina maana gani?
A. Malipo
B. Malipo kwa kusababishiwa hasara
C. Mahari
D. Makato ya pesa
E. Fedha za mkataba

iii. Mama alisema mtoto aliyepotea amepatikana akiwa hai. Je, hii ni aina gani ya sentensi?
A. Shurutia
B. Changamano
C. Ambatano
D. Sahili
E. Tata

iv. Baba amenunua nguo zilizotengenezwa ya _________ya kondoo.
A. Sufi B. Sufu C. Nyoya D. Zufu E. Nyama

v. "Unapenda mchezo gani? Dada aliuliza. Hii ni kauli gani?
A. Tamati B. Awali C. Taarifa D. Halisi E. Mbiu

vi. Tulimuona mamba akitembea kiupandeupande. Je, kielezi katika sentensi hii ni kipi?
A. Akitembea B. Tulimuona C. Mamba D. Upande upande E. Akitembea kiupande

vii. Kilomondo si tajiri sana hapa kijijini. Neno "si" limetumika kama aina gani ya neno?
A. Nomino B. Kielezi C. Kitenzi D. Kivumishi E. Kihisishi

viii. Mgeni rasmi aliwasili saa tisa alasiri. Tungo hii ipo katika wakati gani?
A. Ujao B. Uliopita C. Mtimilifu D. Mazoea E. Uliopo

ix. Bainisha kivumishi katika sentensi ifuatayo"Juma na Roza ni wanafunzi hodari sana wawapo darasani".
A. Roza B. Ni C. Wanafunzi D. Na E. Hodari

x. Alisema kuwa hawezi kuongozana na ninyi. Badili sentensi hii kuwa kauli halisi.

A. Nimesema siwezi kuongozana nao
B. Siwezi kuongozana na ninyi
C. Alisema hawezi kuoongozana na ninyi
D. Hatuwezi kuongozana na ninyi
E. Sitaweza kuongozana na ninyi

**3. Oanisha maneno ya kifungu A na yale ya kifungu B ili kuleta mantiki kwa kaundika herufi ya jibu sahihi kutoka kifungu B katika mabano uliyopewa.**

| KIFUNGU A | MAJIBU | KIFUNGU B |
|---|---|---|
| i. Wewe | | A. Nafsi ya pili |
| ii. Kitendo pia nomino | | B. Nafsi ya tatu |
| iii. Kauli taarifa | | C. Penda |
| iv. Wao | | D. Tamaa |
| v. Haba na haba hujaza kibaba | | E. Alisema njoo hapa |
| | | F. Njooni haraka |
| | | G. Chembe na chembe mkate huwa |
| | | H. Ngoja ngoja yaumiza matumbo |

**SEHEMU B:**

**4. Sentensi zifuatazo zimechanganywa, zipange kwenye mtiririko wenye mantiki kwa kutumia herufi A, B, C, D na E.**

i. Wazazi wanaitwa Lisa na Bishanga. __________
ii. Wananihimiza kila siku kuwa na matumizi mazuri ya mtandao. _________
iii. Mimi naitwa Joti. ________
iv. Hakika mola awajalie maisha marefu. ________
v. Licha ya kuwa ni wazee ila wanaijua vema Sayansi na Teknolojia. _______

**5. Soma shairi lifutalo kisha jibu swali i-v kwa kuandika jibu sahihi**

1. Ungeyatoa machozi, kuliko kutabasamu,
Unadhani ni azizi, kuweka kando elimu,
Kijana acha ubozi, usomesome kwa hamu,
Hakika elimu muhimu, katika hii dunia.

2. Nakwambia waziwazi, elimu kitu adimu,
Ukifanya laazizi, akilini itadumu,
Epuka wanobarizi, dukani kama sanamu
Hakika elimu muhimu, katika hii dunia.

3. Yasafishe masikizi, ubongo uwe timamu,
Shuleni uchape kazi, pamoja nao hirimu,
Kubaki kwenye gonezi, dunia takudhulumu,
Hakika elimu muhimu, katika hii dunia.

4. Mtindo wa siku hizi, kusoma na kufahamu,
Soma sifanye ajizi, elimu kweli ni chumu,
Una akili tambuzi, daima uiheshimu,
Hakika elimu muhimu, katika hii dunia.

**Maswali**

i. Unadhani kirefu cha neno "wanobarizi? Kama lilivyotummika katika shairi hili ni kipi?
_______________

ii. Malenga ametumia muundo upi kutunga shairi ulilolisoma?
_______________

iii. Mkarara wa shairi hili una mizani mingapi? _______________

iv. Kwa mujibu wa shairi ulilolisoma unafikiri ni kipi chafaa kuwa kichwa cha shairi kilichobeba ujumbe uliokusudiwa? _______________

v. Andika vina vya ndani na vya njee vya shairi hili _______________ na _______________

**SEHEMU C**

6. **Tumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku kujibu swali la 36 – 40 kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.**

| |
|---|
| **Saini ya mwandishi, Kumbukumbu namba, Kichwa cha barua, Tarehe, Anuani ya mwandishi** |

i. _______________

ii. _______________

iii. _______________

Mwalimu Mkuu,

Shule ya msingi Azimio,

S.L.P 57,

Urambo

Ndugu,

iv. _______________

Tafadhali husika na somo lillo hapo juu.

Mimi ni mwanafunzi wa darasa la saba katika shule yako. Ni heshima yangu kukuandikia barua hii kukujilisha kuwa, nimepatwa na msiba, hivyo itanilazimu kuchelewa kurudi shuleni ili niweze kuhudhuria mazishi ya marehemu bibi yangu. Kwa barua hii naomba nitoe taarifa kuwa nitarejea shuleni wiki ijayo siku ya Jumatatu.

Natanguliza shukrani kwa kunielewa

Wako mtiifu,

v. _______________

Daudi Dalali

## UFAHAMU WA KUSIKILIZA

Siku moja katika uchaguzi wa viongozi wa Kijiji cha Songambele, kilichopo kata ya Muungano. Watu wengi walijitokeza kugombea nafasi mbalimbali. Miongoni mwa waliojitokeza kugombea nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji ni mzee Lukuminga, mzee Mtasha, mzee Mdula na kijana mmoja aliyefahamika kwa jina la Maganga, aliyetokea katika familia duni tena asiye maarufu kama walivyokuwa wagombea wenzake. Wengi walimshangaa kijana Maganga kuamua kushindana na wazee vigogo na maarufu katika Kijiji. Lakini yeye alikuwa ni kijana jasiri na mwenye msimamo asiyependa mzaha katika kazi. Hakuwa na lugha za kubembeleza hasa kuhusiana na kufanya kazi kwa juhudi. Alieleza kinagaubaga kuwa ikiwa atachaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kijiji atasimamia watu kufanya kazi kwa bidii ili wajitafutie maendeleo yao wenyewe na pia atasimamia mapato na matumizi ya Kijiji kwa uwazi ili kuwakomesha wale wote wanaotumia mianya hiyo kufanya usifadi. Mungu si Athumani kutokana na sera zake hizo watu wengi walimkubali. Baada ya kura kupigwa na kuhesabiwa, msimamizi wa uchaguzi bwana Jumbe alitangaza kuwa Maganga ameibuka kidedea na kutawazwa kuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Songambele.